**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIDETE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 0653 984 226**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0789 015 045**

**Matron: 0714 183 004**

**Shule ya Sekondari: Kidete**

**S.L.P 36078**

**Tarehe: 16/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIDETE HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI MKOA DAR ES SALAAM MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2024** na atasoma tahasusi ya ……..……....na Shule itafunguliwa rasmi tarehe**1/07/2024** na mwisho wakuripoti ni tarehe **30 /08/2024.**

Shule ipo mkoa wa **Dar es Salaam**, Wilaya ya **Kigamboni**. Kata ya **Mjimwema. Kwa** wanaotoka mikoani washuke kituo kikuu cha mabasi **MBEZI**. Wapande mabasi ya mwendo kasi yanayoelekea **Kivukoni**. Baada ya kufika **Kivukoni** avuke maji kwa kutumia Panton (ferry) baada ya kuvuka aelekee stendi ya daladala za Kigamboni apande daladala za kuelekea **CHEKA**. zimeandikwa **Kigamboni –Cheka** ashuke **Kibugumo** kituo kinachoitwa **Kibugumo Shule**. Ukishuka hapo shule ipo upande wa kushoto umbali wa nusu kilomita kutoka barabara ya kuu (Lami.)

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) za draft ya rangi ya maruni na kijivu. Mshono ni **SKETI YA "V"** yenye mifuko miwili, urefu sentimita 35 kutoka kwenye magoti na isiyobana mwili. **(Sampuli ya rangi ya kitambaa cha sketi na aina ya mshono imeambatanishwa katika kiambata "A na "B").**

ii. Mashati mawili (2) mikono mirefu rangi nyeupe aina ya tomato pamoja

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni juba na nusu kanzu nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama .

iv. Sare ya Michezo ni jezi rangi ya maruni.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vii. Sweta moja ya rangi ya maruni mshono wa V .

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*), gauni ya dark blue mshono wa solo yenye urefu wa sentimeta 35 kutoka kwenye magoti (kitambaa cha suti namba moja) ambazo zitavaliwa muda wote awapo bwenini na juba la cream kwa wanaovaa hijjab. (**Sampuli ya Kitambaa cha Gauni la kushindia pamoja na aina ya mshono vimeambatanishwa katika viambata "C" na "D")**

ix. Tai ni rangi inayofanana na sketi.

x. Tisheti (T-shirt) form six rangi ya maruni inavaliwa Jumatano na Tshirt nyeupe (round colar) inavaliwa ijumaa. (Zinapatikana shuleni)

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa (Counter Book quire 3) daftari 8

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*Orodha ya vitabu kwa kila Tahasusi imeandikwa fomu namba 4 ukurasa namba 13*);

iv. Scientific Calculator;

v. Godoro la wanafunzi liwe na vipimo futi 2.5 kwa futi 6.

vi. Mashuka Jozi 2 (moja rangi ya **Pink** na jingine rangi ya **Light blue**), blanket 1, foronya ya godoro (moja rangi ya Pink na nyingine rangi ya Light blue), chandarua 1 ( *futi nne kwa sita(4x6))*

vii. Aje na nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Wanafunzi wa **HGK** waje na kwanja na fagio la ndani na wanafunzi wa **HKL** waje na Jembe na mopa.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**ANGALIZO:**

- Michango yote (**Tshs 80,000/=)** itumwe kwenye akaunti namba **20101100239** benki ya NMB kwa jina na akaunti **KIDETE SECONDARY SCHOOL. Zingatia kuandika jina kamili la mwanafunzi na tahasusi yake unapotuma mchango wake na mwanafunzi aje na slip ya malipo anaporipoti shuleni.**
- **Tunashauri pia mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA, ili kupunguza gharama za matibabu kwa mzazi.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0653984226**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0789015045**
- **Mwandamizi Taaluma : 0614819000**
- **Mwandamizi Malezi : 0714 183 004**

**VIAMBATA**

KAMBATA – "A" (**RANGI YA SKETI YA SHULE NA MSHONO**)



KIAMBATA “C”: **RANGI YA KITAMBAA CHA GAUNI LA KUSHINDIA NA MSHONO. (DARK BLUE)**



## FOMU NAMBA 1

**FOMU YA USAJILI KWA MWANAFUNZI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI).**

PICHA YA MWANAFUNZI

**SEHEMU "A" IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE.**

1. Jina kamili la Mwanafunzi ……………………………..
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………….
3. Mahali (Wilaya)……………………………..
4. Uraia……………………………….
5. Dini ……………………Dhehebu……………………………….
6. Shule ya Sekondari uliyosoma(F. IV)…………………………
7. Namba ya Mtihani.………………….......................................
8. Mahali unapoishi kwa sasa……………………………………

PICHA YA MZAZI/MLEZI

**AHADI YA MWANAFUNZI:**
Mimi Nakubali nafasi niliyopewa ya Kidato cha**………….**
Naahidi kutii kikamilifu Sheria / Kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa KIDETE SEKONDARI
**SAHIHI YA MWANAFUNZI………………………..**
**TAREHE…………………..**

**SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI / MLEZI:**

i. Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………………………………
ii. Kazi……………………………………………………………………
iii. Anuani ……………………………………………………………
iv. Simu…………………………………………………………………...
v. Mahali ninapoishi……………………………………………………..

**FOMU NAMBA 2**

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

### SHULE YA SEKONDARI KIDETE

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ……………………………………………………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………………(tarehe , mwezi mwaka)
3. Kabila ……………………………………………………Taifa ………………………………………………………………
4. Dini na madhehebu ……………………………………………………………………………………………………
5. Jina la baba …………………………………………………………………………Taifa ……………………………
6. Anuani ya baba………………………………………………………………………………………………………………
7. Kazi ya baba………………………………………………………………………………………………………………..
8. Jina la mama………………………………………………………………………………………………………………….
9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana ………………………………………………………………….
10. Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea Shuleni :

| S/N | JINA LA MZAZI | UHUSIANO | SIMU NAMBA | ANAKOISHI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi (taja sehemu moja tu utakayokwenda kila wakati na anuani …………………………………………………………………………………………………….
12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi
    Sahihi ya mwanafunzi ……………………………… Tatehe …………………………………………

Sahihi mzazi/mlezi ……………………………………Tarehe ……………………………

**FOMU NA 3:**

**FOMU YA TAARIFA YA AFYA YA MWANAFUNZI "MEDICAL EXAMINATION FORM"**

**Maelezo**: Fomu hii ijazwe na Mganga Mkuu wa Mkoa /Wilaya / Kituo cha Afya na Mwanafunzi aje nayo shuleni na kuikabidhi ofisi ya nyaraka za wanafunzi.

Mimi [Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya] …………………………….…………
Nathibitisha kuwa………………………………………… [Jina la mwanafunzi]
Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana anayo / hanayo afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;-

**B) Hali ya mwili**

i) Mapigo ya moyo…………………………………………………….
ii) Haemoglobin ……………………………………………………..
iii) Kundi la damu [blood group]…………………………………….
iv) Mkojo (Urine)…………………………………………………....
v) Kinyesi (Stool) ……………………………………………………..
vi) Macho yana kasoro……………………………………………..
vii) Masikio yana kasoro……………………………………………..

**Angalia**: Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (**i**)-(vii)

**C) Magonjwa**

i) Bronchial asthma……………………………………………………..
ii) Tuberculosis…………………………………………………………
iii) Epilepsy……………………………………………………………..
iv) Blood pressure…………………………………………………
v) Peptic/duodenal ulcers……………………………………
vi) Sickle cells…………………………………………………..
vii) Leprosy…………………………………………………
viii) Venereal disease [give type……………………………]
ix) Mental illness………………………………………………
x) Any other serious disease not mentioned above…………………………………………………………..

**SAINI YA DAKTARI…………………………..TAREHE……………………… MUHURI ………………**

## OORODHA YA VITABU

Orodha ya vitabu vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Kila mwanafunzi anatakiwa kununua baadhi ya vitabu hivyo kwa kila somo kwa masomo aliyopangiwa yaani **HGK** (History, Geography na Kiswahili au **HKL** (History, Kiswahili na English Language). General studies ni kwa wote.

### 1. HISTORY

a) TIE (2022) History for Advance Secondary School Students Book Form Five. Tanzania Institute of Education.
b) Yasini S (….) Essential in Advance Levels History Paper One.
c) Bakari Madaya (….).History Paper One, Lesson Notes for Advance Certificate of Secondary Education.

### 2. ENGLISH LANGUAGE

a) Asheri, N.(2014) Advanced Level English: A Practical Approach,8TH Ed., Dar es Salaam: Good Books Publishers.
b) John, J. (2012) Advanced English Language: Form 5 & 6, Dar es Salaam: Oxford University Press.
c) TIE (2016) English Language for Secondary Schools: Literature and Stylistics Form Five and Six, Dar es Salaam: Tanzania institute of Education

### POETRY

(a) Selected Poems. - Tanzania Institute of Education
(b) The wonderful Surgeon and Other Poems. – Charles Mloka - Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

### PLAYS

(a) Betrayal in the City - Francis Imbunga
(b) I Will Marry When I Want - Ngugi wa Thiong’o and Ngugi wa Mirii
(c) Lwanda Magere - Okoiti Omtatah
(d) An Enemy of the People - Henrik Ibsen
(e) Black Mamba - John Ruganda

### 3. GEOGRAPHY

a) Geography for Secondary Schools: Form Five. - Tanzania Institute of Education (2016)
b) Practical Geography: Map-reading, Photograph, Research and Surveying. – Zisti Kamili
c) Geography Review

d) Geography Coloured map sheets and Photographs
e) Scientific Calculator fx 991
f) R.B Bunnet (1997) Physical geography and diagrams
g) Kothari O.R (2009) Research methodology, methods and techniques 2nd Edition

**4. KISWAHILI**

**(i) KISWAHILI 1**

a) Nadharia ya lugha ya Kiswahili1: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangwine na Masebo - (2010)
b) Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B: TUKI (2003)

**(ii) KISWAHILI 2**

a) Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita – Masebo – Oxford university Press
b) Tahakiki Vitabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangwine na Masebo

**TAMTHILIA (walau vitabu viwili)**

1) Kivuli Kinaish – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press
2) Kwenye Ukingo wa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
3) Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)
4) Morani –Emanuel Mbogo (1993)

**RIWAYA (walau vitabu viwili)**

1) Vuta ni Kuvute, 4th ed. – Mbunda Msokile (2009)
2) Kufikirika, 4th ed. – Shaban Robert – Mkuki na Nyota
3) Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
4) Usiku Utakapokwisha, 2nd ed. – Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

**USHAIRI (walau vitabu viwili)**

1) Kimbunga: Toleo la Tatu (3rd ed.) – Haji Gora Haji (1995) - TUKI
2) Chungu Tamu – Theobald Mvungi
3) Mapenzi Bora – Shaban Robert – Mkuki na Nyota publishers
4) Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan

5. **GENERAL STIUDIES**

1. Nyangwine, C.M, Bukagile G.R & Maluka S.O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies Notes form 5 & 6.